# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
# MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA SITA

**121/2**

## KISWAHILI 2

(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 3** **Mwaka: 2025**

---

### Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **nane (8)**.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na maswali **matatu** (3) kutoka sehemu B. Swali la **tano (5)** ni la lazima.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Zingatia maagizo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
5. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa **bluu** au **mweusi**.
6. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
7. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

2 502121 200010

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Maendeleo ya sayansi na teknolojia yameifanya fasihi simulizi kupoteza uhalisia katika uwasilishaji wake. Tathmini kauli hiyo kwa kutoa hoja tano zenye mifano.

2. "Mhakiki ni msanii aliyebobea katika nadharia, misingi na utendaji wa taaluma ya utunzi." Fafanua kauli hiyo kwa kutoa hoja tano.

3. Elezea dhana za kifasihi zifuatazo:
   (a) Mafumbo
   (b) Lakabu
   (c) Misemo
   (d) Nahau
   (e) Mizungu

4. Soma matini ifuatayo, kisha bainisha vipengele vya kifani vilivyotumika:

Bwana Majivuno, Meneja wa Kampuni, mtafuna mali za umma; alijiona kuwa umma umekubali kumpokea. Akaanza kujisifu kuwa, kati ya mameneja wote nchini, yeye ndiye aliyejua shida za wananchi peke yake. Kumbe bwana, "Waswahili wamejawa na busara." Kwa nini nasema hivyo? Nasema hivyo kwa kuwa waswahili husema kuwa, "Adhaniaye amesimama aangalie asianguke." Mzee wangu bwana Bubase aliwahi kuniambia kuwa, ukiona mtu haridhiki na cheo chake, ujue huyo ni rahisi kununuliwa na kuisaliti jamii.

Huyu ndiye alikuwa bwana Majivuno, ambaye ni paka-shume ofisini kwake, mtaani kigogo na fataki. Nyumbani je? Nyumbani kwa watoto ni simba. "Aungurumapo simba, mcheza nani?" Ha! Haa! Haaa! Ule ucheshi wake wa ofsini haukuonekana kwa mabinti zake kumi na tatu aliokuwa nao. Jamaa alikuwa jemadari kweli asiye na mchezo. Watoto wake walizoea kumuita "Mdingi," wakisikia gari nje, unasikia wanaambizana...Mdingi anaingia...wote hufyatukia vyumbani mwao fyuuuuuuu!

Bwana Majivuno alitoa amri kuwa mabinti wake wote wawe wamerudi nyumbani ifikapo saa kumi kamili jioni, na wasitoke tena! Sasa hapo ndipo nawaungamia tena waswahili kwa kusema kuwa, "Mkuki kwa nguruwe mtamu, kwa binadamu ni shubiri." Alikuwa bonge la "fataki" kwa mabinti wa wenzake huku kwa wa kwake akiwa pilipili. Kila siku asubuhi, watoto wake wote hupita kwa mstari kutoa "shikamoo"...ole wake asiyepita. Anakinukisha asikwambie mtu. Usiku kabla ya kulala hivyo hivyo shikamoo lazima imtembelee bwana huyu; yeye akiwa amekaa kwenye kochi huku akiwa kifua wazi, tumbo nje kama kiroboto.

Wakati wa kula, Majivuno alizoea kukohoa; siyo kikohozi cha ugonjwa, bali kikohozi cha kuonesha uzito wa mamlaka aliyonayo. Kikohozi hiki kiliwadokeza kuwa huyu ndiye mwenye ukuu na enzi kwenye nyumba hii. Kila anapokohoa mabinti wake sharti waitikie, "Ewaaaa!" ....Ole wako kwa atakayekosa kuitikia.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

Akiwa nyumbani aliweza kuongea na mke wake tu, labda kwa kuwa waswahili hawakusahau kusema kuwa, "Siri ya mtungi aijuaye kata." Utasikia anaita mke wake "Majivuno"....Naye huitikia "Labeka mke wangu." Pamoja na kuwa aliweza kuongea na mke wake, lakini mara zote ilikuwa ni kutoa amri tu, huku mkewe akifurukuta kwa kuzipangua na kumpa makavu yake.

Siku moja mke wake alimwambia, "Mume wangu wacha kula mali ya umma. Utafungwa!" Majivuno akajibu, "nimekula kuku mzima peke yangu sembuse.........Majivuno hunijui nilivyo simba siguswi, sisogelewi". Labeka akaendelea kumwambia, "zee zima, cheo kikubwa bado mtaani linaitwa "fataki." Majivuno naye akajibu, "mwanaume huachana na matata yake kaburini." Kisha akatoa amri, "Niletee bia haraka!" "Siendi! Na sitaki tabia za kunywa kunywa pombe ovyo! Nakwambia leo hunywi! Umenisahau ee..?"

Huyu ndiye Majivuno, Meneja wa Kampuni, Ofisini paka-shume, mtaani kigogo na fataki, nyumbani kwa watoto simba. Vipi mkewe?

## SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka sehemu hii. Swali la **tano (5)** ni la lazima.

### ORODHA YA VITABU

**USHAIRI**

| | | |
|---|---|---|
| **Kimbunga** | - | Haji Gora |
| **Mapenzi Bora** | - | Shabani Robert |
| **Chungu Tamu** | - | Theobald A. Mvungi |
| **Fungate ya Uhuru** | - | Mohamed S. Khatibu. |

**RIWAYA**

| | | |
|---|---|---|
| **Usiku utakapokwisha** | - | Mbunda Msokile |
| **Kufikirika** | - | Shabani Robert |
| **Mfadhili** | - | Hussein Tuwa |
| **Vuta N'kuvute** | - | Shafi Adam Shafi |

**TAMTHILIYA**

| | | |
|---|---|---|
| **Kwenye Ukingo wa Thim** | - | Ebrahim Hussein |
| **Morani** | - | Emmanuel Mbogo |
| **Kivuli Kinaishi** | - | Said Mohamed |
| **Nguzo Mama** | - | Penina Muhando |

5. Jamii inapokosa maadili ni sawa na nyumba iliyojengwa pasipo msingi imara. Fafanua rai hii kwa kutoa hoja nne kutoka katika diwani mbili ulizosoma.

6. Watunzi wa mashairi ni weledi wa kuteua mandhari yenye uwezo wa kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Tathmini ukweli wa kauli hii kwa kutoa hoja tatu kwa kila kitabu katika diwani mbili ulizosoma.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

7. "Mtindo ni upekee wa mwandishi katika uandishi wa kazi za fasihi." Kwa kutumia riwaya mbili ulizosoma, toa hoja tatu kwa kila riwaya ukionesha jinsi mtindo wa riwaya hizo unavyofanana na unavyotofautiana.

8. Suala la ukombozi ndio kilio kikuu cha waandishi wengi katika karne ya ishirini na moja. Pendekeza mbinu nne zilizotumiwa na waandishi katika kufikia ukombozi halisi kwa kutumia tamthiliya mbili ulizosoma.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner